AFRIPRISE INVESTMENT PLC.

# TAARIFA

## YA MKUTANO MKUU WA 20 WA WANAHISA

Kampuni inapenda kuwajulisha Wanahisa wote kuwa Mkutano Mkuu wa Ishirini wa Wanahisa wa Kampuni ya Uwekezaji ya **AFRIPRISE** utafanyika siku ya Jumamosi, tarehe 15/11/2025, kuanzia saa 3:00 Asubuhi, kwa njia ya mtandao. Wanahisa wote watapokea maelekezo ya kujiunga na kushiriki Mkutano kupitia ujumbe wa simu au barua pepe, pamoja na kiungo cha Mkutano.

### DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI (KWA AJILI YA MWAKA WA FEDHA 2024):

1. Kufungua Mkutano Mkuu wa Ishirini
2. Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa
4. Kujadili Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa
5. Kupokea, kujadili na kuridhia:
    a. Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi
    b. Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji
    c. Taarifa ya Wakurugenzi Pamoja na Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2024
6. Kupokea, Kujadili na kuridhia Pendekezo la Gawio kwa mwaka wa fedha 2024
7. Kupokea, kujadili na kuridhia Pendekezo la uteuzi wa Mkaguzi wa nje wa Mahesabu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2025
8. Kupokea, kujadili na kuridhia Pendekezo la Malipo ya Wajumbe wa Bodi kwa mwaka, 2025
9. Kupokea, Kujadili na Kuridhia Pendekezo la Utoaji wa Hisa za upendeleo zisizo na Haki ya Kupiga Kura zenye Uwezo wa Kukombolewa (Non-Voting Redeemable Cumulative Preference Shares)
10. Kupokea na Kujadili mapendekezo rasmi yaliyowasilishwa na Wanahisa
11. Kufunga Mkutano Mkuu

### MAELEZO MUHIMU KWA WANAHISA:

1. **Mapendekezo toka kwa Wanahisa:** Wanahisa wanahimizwa kuwasilisha mapendekezo yao kwa maandishi kwa Katibu wa Kampuni kabla ya tarehe 10/11/2025 ili yaweze kujumuishwa katika Dondoo namba 10 ya Mkutano.
2. **Taarifa ya Mwaka na Makabrasha:** Taarifa ya Mwaka 2024 pamoja na Makabrasha ya Mkutano yatapatikana kwenye tovuti ya Kampuni kuanzia tarehe 01/11/2025 kupitia anwani: *https://www.afriprise.co.tz*
3. **Uwakilishi:** Kama Mwanahisa hataweza kuhudhuria Mkutano, anaombwa kuteua mwakilishi kwa kujaza Fomu ya Uwakilishi inayopatikana kwenye tovuti ya Kampuni www.afriprise.co.tz. Fomu zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe: info@afriprise.co.tz au kwa WhatsApp namba: 0757-138048, kabla ya tarehe 14/11/2025, saa 10:00 jioni.

Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi

**Peter W. Kifunguomali**
Katibu wa Kampuni